

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



BARABARA RA HASSAN NGWILIZI
S.L.P. 1953,
21105 TANGA
Simu Nambari: 027-2645186,
Nukushi: 027-2647885
Barua Pepe: rbctanga@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz
TANZANIA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TANGA MEI 10, 2019

AFISA MTENDAJI KIZIMBANI KWA RUSHWA

Aliomba kupelekewa usiku apelekewe fedha usiku mwingi, TAKUKURU ikamdaka

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tanga, leo tarehe 10/05/2019 itamfikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Korogwe IDRISA MOHAMED SHELUKINDO, ambaye ni Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kwa wadhifa wa Afisa Mtendaji wa Serikali ya Mtaa wa OLD KOROGWE kwa makosa ya rushwa.

Bw. IDRISA MOHAMED SHELUKINDO anashtakiwa kwa makosa mawili Chini ya Kifungu cha 15 (1)(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007. Katika kosa la kwanza huko wilayani Korogwe kwa nyakati tofauti za mwezi wa April, 2019 hadi hadi tarehe 14/04/2019 Bw.IDRISA MOHAMED SHELUKINDO aliomba apewe Rushwa ya kiasi cha fedha za kitanzania **Laki Tano tu** (500,000/=) kutoka kwa Bw. LONGINUS MELKION NCHIMBI ili aweze kumsaidia asifikishwe Mahakamani na Polisi kwa kosa la kufanya Biashara ya ukopeshaji fedha bila ya kuwa na leseni ya kufanya biashara hiyo.

Awali, Afisa Mtendaji huyo alikuwa amemkata Bw. LONGINUS na kumfikisha Polisi kwa kuendesha biashara hiyo ya ukopeshaji wa fedha kinyume cha sheria.

Kosa la pili linalo mkabili Bw.IDRISA MOHAMED SHELUKINDO ni kwamba mnamo tarehe **14/04/2019** akiwa Mtumishi wa halmashauri ya Wilaya ya Korogwe mwenye wadhifa au Cheo cha Afisa Mtendaji wa Mtaa alikubali kupokea Rushwa ya kiasi cha fedha za kitanzania **Shilingi Laki Mbili tu (200,000)** ili aweze kumsaidia asifikishwe Mahakamani na Polisi kwa kosa la kufanya Biashara ya ukopeshaji fedha bila ya kuwa na leseni ya kufanya biashara hiyo.

WITO

Tunawaomba wananchi wa Mkoa wa Tanga na wadau wote katika Mapambano Dhidi ya Rushwa mwendelee kushirikiana na Taasisi yenu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) bila ya uoga katika kufichua na kuta taarifa za vitendo vya rushwa. TAKUKURU tupo kazini pamoja nanyi siku zote, masaa yote na mahali popote. Tukiungana katika Mapambano Dhidi ya Rushwa hakika watanzania tutaiona thamana ya baraka na utajiri mwingi nchi yetu iliojaaliwa na mwenyezi Mungu.

Aidha, ni ushauri wangu kwa wala rushwa na wapenda rushwa kwamba; watafute namna nyingine halali ya kujipatia ama kujiongezea kipato. Rushwa itawatoa uhai na kuziachia familia zao kumbukumbu ya fedheha maishani.

Imetolewa na:

Christopher J. Mariba

MKUU WA TAKUKURU MKOA WA TANGA.